

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA RUKWA
Anuani ya Simu: "REGCOM"
Simu Na: 025-2802318/2802137
Nukushi. (025) 2802217
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
55180 Sumbawanga,
RUKWA.

TAARIFA KWA UMMA
KONGAMANO LA UWEKEZAJI MKOANI RUKWA LITAKALOFANYIKA KUANZIA
TAREHE 25- 30 MEI 2023

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inawataarifu wananchi wote kuwa imeandaa Kongamano la Uwekezaji Mkoa wa Rukwa litakalofanyika katika viwanja vya Nelson Mandela kuanzia tarehe 25 Mei 2023 hadi tarehe 30 Mei 2023. Shughuli zitakazofanyika katika Kongamano hilo ni pamoja na:

- Maonesho ya bidhaa za Kilimo na Biashara.
- Mdahalo kuhusu uwekezaji utakaofanyika tarehe 29 Mei 2023 kuanzia saa 4.00 Asubuhi katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari Mtakatifu Maurus Chemchem. Watu Mashuhuri, Viongozi wa Serikali na Sekta Binafsi kutoka nchi mbalimbali watahudhuria.
- Kutembelea maeneo ya uwekezaji na utalii mkoani Rukwa.

Wafanyabiashara, Wajasiriamali, Wakulima na Watoa huduma wote mnaalikwa kuitumia fursa hiyo kufanya biashara ,kujitangaza na kukutana na wafanyabiashara wa kimataifa kutoka nchi mbalimbali.Usajili utafanyika kuanzia tarehe 09 -15 Mei,2023 katika Ofisi za Biashara Manispaa ya Sumbawanga.Hakikisha unawasilisha sampuli ya bidhaa unazozalisha kwa ajili ya ukaguzi.

Mgeni Rasmi Katika kongamano hili anatarajiwa kuwa Mhe. Dkt Ashatu Kijaji Waziri wa Viwanda na Biashara. Wananchi wote mnakaribishwa.

Imetolewa na

Khadija Dalasia
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Mkoa wa Rukwa
09 Mei 2023

